

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA**

**121/1**

**KISWAHILI 1**

(Kwa watahiniwa Walioko Shulen na Wasiokuwa Shulen)

**Muda: Saa 3**

**Mwaka: 2020**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenyе jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B.
3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu na ya kila swali**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org



## **SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **vote** katika sehemu hii.

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kwa umakini kisha jibu kwa usahihi maswali yanayofuata:

Sanaa za maonyesho ni sanaa ambazo usuri wake umo katika umbo la vitendo, na ili kupata uzuri huu yampasa mtu kutazama vitendo vinavyofanyika. Umbo hili hulazimishwa kuwepo kwa fanani na hadhira mahali pamoja ama sivyo sanaa haikamiliki. Hali hii ndiyo inayosababisha sanaa hizi za vitendo kuitwa sanaa za maonyesho.

Katika jamii nyingi za kiafrika sanaa za maonyesho ziliweza kutendeka kupertia jando na unyago, majigambo na utani. Wakati mwingine sanaa za maonyesho zilikuwa zinajitokeza ndani ya hadhithi mbalimbali zilizobuniwa na mababu, ngoma, matambiko, michezo ya watoto pamoja na mivigha.

Jamii bora ilitambulika kutokana na sanaa za maonyesho. Katika sanaa za maonyesho kulikuwa na mitaala maalumu kama ilivyo leo na sanaa hizi ziliweza kufanya kazi ya mwalimu na mwanafunzi katika darasa maalumu.

Sanaa za maonyesho ni kitovu cha utamaduni wa mwafrika. Katika zama za kale, sanaa za maonyesho **zilifanya** sana. Mababu na mabibi waliketi pamoja kila jioni na wajukuu zao na kuwasimulia hadithi pamoja na kuimba nyimbo mbalimbali. Sanaa za maonyesho zililenga katika kuwakuza vijana wawe na maadili mema na kuwaandaa kushiriki majukumu mbalimbali, uzalendo, ujasiri, ushujaa na kuwa raia wema wa siku zijazo. Wakati huo watu waliishi kwa umoja na kupendana. Watu walifanya kazi pamoja na kugawana matunda ya kazi kwa usawa. Hapakuwa na ubinagsi. Kila jambo lilifanyika kwa maslahi mapana ya wanajamii wote. Sanaa za maonyesho zilifanyika muda wa jioni kwa lengo la kujiburudisha na kujipongeza kutokana na kazi za mchana kutwa.

Utaratibu huu wa maisha uliendelea mpaka **majilio** ya wakoloni. Wakoloni walipovamia na kuligawa bara la Afrika hawakupenda kuona utamaduni wa waafrika unaendelea **kutamalaki**. Hivyo, sanaa za maonyesho zilianza kusakamwa na wakoloni na walihakikisha wanatumia mbinu mbalimbali ikiwezekana zipotee kabisa. Walipiga marufuku upigaji wa ngoma na nyimbo nyakati za usiku. Walipinga jando na unyago kwa kuanzisha elimu yenye mkondo wa zikabadilika kadiri ya maingiliano na watu na **utandawazi** ulipokuwa unashika kasi. Maendeleo ya sasa ya sayansi na teknolojia yanaendelea kuathiri utendaji na ufanyakaji wa sanaa za maonyesho. Pamoja na changamoto hizo bado wito unaendelea kutolewa wa kulinda sanaa zetu za jadi na kuendeleza utamaduni na hatimaye kurithisha kwa vizazi vijavyo.

## **Maswali**

- (a) Andika kichwa cha habari uliyosoma kisichozidi maneno matatu.
- (b) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivytumika katika habari uliyosoma:  
. (i) Zilifana  
(ii) Majilio  
(iii) Kutamalaki  
(iv) Utandawazi
- (c) Kutokana na habari uliyosoma, taja manufaa matatu ya sanaa za maonyesho.
- (d) Mwandishi ana maana gani anaposema, “Sanaa za maonyesho zilifanya kazi ya mwalimu na mwanafunzi katika darasa maalumu?”
2. (a) Fasili neno rejestra.  
(b) Kwa kutumia mifano, fafanua matumizi manne ya rejestra.
3. Toa maana za istilahi zifuatazo kama zinavyotumika katika lugha ya Kiswahili.  
(a) Sarufi.  
(b) Mzizi wa neno.  
(c) Sarufi maumbo.  
(d) Sarufi matamshi.  
(e) Sauti miundo.
4. (a) Tumia -O- rejeshi kuandika upya sentensi zifuatazo:  
(i) Aliingia mahali mna chatu.  
(ii) Alighani shairi zuri sana.  
(iii) Alinunua kiti kibovu.  
(iv) Alivunja nazi mbovu.  
(v) Alipata ugonjwa ambao haujulikani.
- (b) Weka nomino zifuatazo katika ngeli husika kwa kigezo cha kisintaksia  
(i) Mahali  
(ii) Shairi  
(iii) Kiti  
(iv) Nazi  
(v) Ugonjwa

## **SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swalii la **nane (8)** ni la lazima.

5. Rafiki yako aitwaye Sikudhani Tumaini anatarajia kufunga ndoa mwezi Juni. Andika kadi ya kuomba mchango wa harusi hiyo inayotarajia kufanyika tarehe 15/6/2020.
6. Kwa kutumia mifano, bainisha mambo sita yanayosaidia kukua na kuendelea kwa Kiswahili duniani.
7. Tathmini upungufu uliojitokeza wakati wa kusanifisha Kiswahili kabla ya uhuru. Toa hoja sita.
8. Fafanua changamoto tano zinazojitokeza katika kufasiri matini za Kifasihi.